PUBLIC PROCUREMENT APPEALS AUTHORITY
Efficient and Fair Appeals Dispensation
PPAA
MAMLAKA YA RUFANI YA ZABUNI ZA UMMA

PPAA
Toleo Na: 03 Oktoba - Desemba 2024

# BULLETIN

UTOAJI RUFAA KWA UFANISI NA HAKI



*Katibu Mtendaji - PPAA*
*Bw. James Sando*

## Falsafa ya R4 za Rais Samia nguzo kuimarisha utoaji haki

**Mpendwa msomaji** karibu tena ujisomee toleo la tatu la Jarida la Mtandaoni kutoka Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA).

Katika jarida hili utapata fursa ya kusoma na kupata uelewa wa majukumu na huduma zinazotolewa na PPAA pamoja na jinsi Mamlaka ya Rufani inavyotumia falsafa ya R4 za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kuimarisha utoaji haki, kuongeza uwazi na uwajibikaji katika zabuni za umma.

Aidha, kupitia Jarida hili utafahamu majukumu mbalimbali yaliyotekelezwa na PPAA kwa kipindi cha miezi mitatu (Oktoba – Desemba, 2024) katika kuhakikisha Mamlaka ya Rufani inatoa rufaa kwa ufanisi na haki.

Toleo hili ni muendelezo wa matoleo mawili yaliyopita ambapo pamoja na mambo mengine, limelenga kukuhabarisha kuhusu shughuli mbalimbali za Mamlaka ili kuongeza tija ya kuwahabarisha wadau wa ununuzi na wananchi kwa ujumla.

Karibu tena usome jarida hili ili ufahamu kwa undani PPAA na shughuli mbalimbali ilizozitekeleza katika kipindi cha miezi mitatu (Oktoba – Desemba, 2024).

***#Kazi Iendelee.***

# PPAA yaokoa bilioni 583.5/- michakato zabuni za umma

**MAMLAKA ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) imefanikiwa kuzuia upotevu wa fedha za serikali takribani TZS. 583,591,615,609.00 katika mashauri 162 yaliyokuwa katika hatua mbalimbali za michakato ya ununuzi wa umma kwa kipindi cha miaka takribani miaka minne.**

Hayo yalibainishwa na Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando alipozungumza na waandishi wa habari pembezoni mwa Kongamano la 15 Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi katika viwanja vya Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha (AICC), jijini Arusha.

"Katika kipindi cha takribani miaka minne tumeweza kusikiliza mashauri 162 na baada ya kupitia mashauri hayo, tumezuia zabuni 35 zenye takribani bilioni 583.5/- ambapo endapo zabuni hizo zingetolewa kwa wazabuni hao waliokosa sifa, zingesababishia Serikali hasara katika eneo hilo," alisema Bw. Sando.

Aidha, Bw. Sando aliongeza kuwa PPAA imekamilisha mchakato




*Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko (Mb.) akihutubia wakati wa ufunguzi wa Kongamano la 15 Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi lililofanyika katika viwanja vya Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha (AICC), tarehe 17 – 19 Desemba 2024, jijini Arusha.*

wa kujenga moduli ya kuwasilisha malalamiko na rufaa kwa njia ya kieletroniki katika mfumo wa Ununuzi wa Umma Kieletroniki (NeST), kinachosubiriwa ni kukamilika kwa Kanuni za Rufaa za Ununuzi wa Umma ambapo zipo katika hatua ya mwishoni.

Pamoja na mambo mengine, Bw. Sando ameongeza kuwa baada ya kukamilika kwa Kanuni Rufaa za Ununuzi wa Umma, PPAA itaendelea na programu ya mafunzo kwa wazabuni na taasisi nunuzi mbalimbali kikanda ili kuwapa uelewa wa kutumia moduli hiyo wakati wa kuwasilisha malalamiko au rufaa kieletroniki.

"Tunategemea kuanza mafunzo ya kutumia Moduli katika Kanda ya Ziwa hususan mikoa ya Mwanza, Kagera, Mara, Shinyanga, Simiyu na Geita na baadae kufuatiwa na mikoa mingine," alisema Bw. Sando.

Aidha, Moduli ya ushughulikiaji wa Malalamiko na Rufaa imewekwa kwenye mfumo wa NeST, uliojengwa chini ya Uongozi wa Serikali ya Awamu

*Inaendelea Uk 2*

BULLETIN
UTOAJI RUFAA KWA UFANISI NA HAKI
PPAA
Toleo Na: 03 Oktoba - Desemba 2024

# PPAA yaokoa bilioni 583.5/-

*Inatoka Uk 1*

ya Sita ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Rais Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Awamu ya kwanza ya mafunzo ya kuhusu moduli ya uwasilishaji wa malalamiko/rufaa kwa njia ya kieletroniki yalifanyika katika mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Morogoro na Pwani na yalifanyika jijini Dar es Salaam tarehe 29 na 30 Mei, 2024.

Awali akifungua kongamano hilo, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko (Mb.) amewataka wataalamu wa ununuzi na ugavi nchini kuwa waadilifu katika utendaji kazi wao sambamba na kukataa rushwa. Dkt. Biteko amesema kuwa Taifa linawategemea sana wataalamu hao katika mahali pa kazi. "Hivyo ni lazima kuhakikisha kuwa mnakuwa waadilifu na nidhamu katika utendaji wa majukumu yenu ya kila siku," alisema Dk Biteko.


BULLETIN

Falsafa 4 za Rais Samia nguzo kuimarisha utoaji haki

PPAA YAOKOA BILIONI 583.5/- MICHAKATO ZABUNI ZA UMMA

BODI YA UHARIRI

Mwenyekiti
Florida Mapunda

Mhariri
Gloria Tesha
Mwandishi wa TSN

Wajumbe
Agnes Sayi
Mohamed Makame
Humphrey Kisanga

Katibu
Nelson Kessy

**Mawasiliano:**
Katibu Mtendaji
5 Mkandarasi Place,
Ghorofa ya nne, 58
Barabara ya Lusinde,
S.L.P. 1385, 41104 Dodoma
Simu: +255 (0) 743505505,
Baruapepe: barua@ppaa.go.tz
es@ppaa.go.tz
Tovuti: www.ppaa.go.tz

# Wataalamu ununuzi wapigwa msasa kuhusu Moduli ya kushughulikia rufaa kieletroniki



*Mkuu wa Sehemu ya Huduma za Sheria za Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), Bi. Agnes Sayi akiwasilisha mada kuhusu matumizi ya moduli ya kuwasilisha na kushughulikia malalamiko na rufaa kwa njia ya kieletroniki kwa wataalamu wa ununuzi na ugavi katika Kongamano la 15 Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi lililofanyika jijini Arusha, tarehe 17 – 19 Desemba, 2024.*

**WATAALAMU wa Sekta ya Ununuzi na Ugavi wamenolewa kuhusu matumizi ya Moduli ya kuwasilisha na kushughulikia malalamiko na rufaa kwa njia ya kielektroniki katika Mfumo wa Ununuzi wa Umma kwa njia ya Kieletroniki (NeST).**

Mkuu wa Sehemu ya Sheria na Huduma za Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) Bi. Agnes Sayi amewasilisha mada kwa wataalamu hao kwa niaba ya Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando wakati wa Kongamano la 15 Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi lililofanyika jijini Arusha, Desemba, 2024.

Pamoja na Mambo mengine, Bi. Sayi aliwanoa wataalamu hao jinsi moduli hiyo inavyofanya kazi hususan katika uwasilishaji na ushughulikiaji wa malalamiko na rufaa kwa upande wa wazabuni pamoja na taasisi nunuzi.

Vipengele vingine ni pamoja na jinsi ya kuwasilisha rufaa nje ya muda, kukazia hukumu na kushughulikia uamuzi uliotolewa kwa kusikiliza upande mmoja.

PUBLIC PROCUREMENT APPEALS AUTHORITY
BULLETIN
UTOAJI RUFAA KWA UFANISI NA HAKI
PPAA
Toleo Na: 03 Oktoba - Desemba 2024

# PPAA yatupilia mbali rufaa ya Dawasa kwa kukosa mashiko

**MAMLAKA ya Rufani ya Manunuzi ya Umma (PPAA) imetupilia mbali rufaa dhidi ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) kwa kukosa mashiko na kuamuru DAWASA kuendelea na mchakato wa zabuni kwa kuzingatia Sheria ya Ununuzi wa Umma.**

Rufaa dhidi ya DAWASA ilifunguliwa na Kampuni ya Ismani Limited baada ya kutoridhika na sababu zilizotolewa za kuondolewa kwenye mchakato wa zabuni wa kuwania zabuni ya usambazaji wa calcium hypochlorite.

Mrufani aliongeza kuwa hakuridhika na kufutwa kwake kwa sababu alikuwa ameweka bei ya chini kuliko Kampuni ya Junaco (T) Ltd aliyeibuka mshindi. Hata hivyo, alishangaa kuona kwamba taarifa ya kusudio la kutoa zabuni ikionesha kwamba DAWASA ilikusudia kumpa zabuni Junaco (T) Ltd ambaye alikuwa na bei ya juu kuliko yeye.

Aidha, Mrufani alieleza kuwa hakuridhika na pendekezo la kumuengua kwenye mchakato wa zabuni. Hivyo, alifanya maombi ya mapitio (administrative review) kwa DAWASA lakini hata hivyo DAWASA ilithibitisha uamuzi wake wa kuonesha nia ya kumpa zabuni Junaco (T) Ltd.

Mrufani alisema kuwa wakati DAWASA wanampa majibu ya malalamiko yake walimueleza kuwa zabuni yake haikukidhi masharti yaliyoainishwa kwenye nyaraka ya zabuni kwa kuwa aliwasilisha dhamana ya benki yenye siku chache ukilinganisha na siku 148 zilizoainishwa kwenye nyaraka ya zabuni.



Kampuni ya Ismani Ltd iliongeza kuwa DAWASA ilipaswa kutoa sababu yenye mashiko kuhusu yeye kuondolewa kwenye mchakato wa zabuni katika barua ya kusudio la kutoa zabuni. Hivyo, kitendo cha DAWASA kuleta sababu mpya ya kufutwa kwa zabuni ya Mrufani wakati wa kushughulikia malalamiko yake kinatia shaka kuhusu uhalali wa mchakato mzima wa zabuni.

Mrufani alifafanua zaidi kwamba, kama DAWASA ilikuwa inajua sababu halali inayomfanya mlalamikaji kuondolewa kwenye mchakato wa zabuni, ingepaswa kujumuishwa katika kusudio la kutoa zabuni. Kitendo cha DAWASA kusema Mrufani aliondolewa kwa sababu ya kutokuwa na bei ya chini katika hatua ya tathmini ya kifedha kinadhihirisha kwamba mlalamikaji alikidhi vigezo vyote isipokuwa vigezo vya bei. Hivyo, Mrufani anaamini kuwa alikuwa na bei ya chini kuliko Junaco (T) aliyeibuka mshindi. Hivyo, kitendo cha DAWASA kumuondoa mlalamikaji katika suala hili kilikiuka sheria.

Ismani Ltd aliongeza kuwa hata kama sababu mpya ya kufutwa kwa zabuni ya mlalamikaji ingekuwa halali, DAWASA ilipaswa kupata ufafanuzi kutoka benki ya CRDB au kwa Mrufani mwenyewe kuhusu tofauti ya muda uliooneshwa kwenye dhamana ya benki kabla ya kuchukua uamuzi wa kumuengua kwenye mchakato wa zabuni.

Kinyume na hayo, DAWASA hakufanya hivyo. Badala yake, alifuta zabuni ya Mrufani na kuendelea kupendekeza kumtangaza mshindi wa zabuni ambaye alikuwa na bei ya juu kuliko ya Mrufani.

Kwa upande wake, DAWASA alieleza mlalamikaji alikuwa miongoni mwa watoa zabuni waliokabidhi zabuni zao kwa hatua za mchakato wa zabuni. Baada ya kumaliza mchakato wa tathmini, zabuni ya Mrufani ilibainika kuwa haikidhi vigezo kwa sababu alikabidhi Dhamana ya Benki yenye siku chini ya 148 kama ilivyoainishwa katika nyaraka ya zabuni.

DAWASA ilisisitiza kuwa kufutwa kwa zabuni ya Mrufani kulikuwa kama ilivyoainishwa kwenye barua yao ya kujibu malalamiko ya mrufani na kama ilivyobainishwa kwenye tathmini ya zabuni. Ila wakati wa kutoa barua ya kusudio ya kutoa tuzo Mfumo ulionesha zabuni ya Mrufani ilifutwa kwa sababu haikuwa zabuni ya bei ya chini katika hatua ya kulinganisha fedha.

DAWASA ilieleza kuwa baada ya kupokea malalamiko ya Mrufani, ilipitia tathmini ya zabuni na kujiridhisha kuwa zabuni ya Mrufani iliengulіwa kwa sababu ya kuwasilisha dhamana ya benki iliyokuwa na siku chache kulinganisha na siku 148 zilizoainishwa kwenye nyaraka ya zabuni. Hivyo sababu halisi ilielezwa kwa Mrufani kwenye barua ya DAWASA iliyojibu malalamiko ya Mrufani.

Kuhusu hoja ya mlalamikaji kwamba kabla ya kuengua zabuni ya Mrufani kuwa haikukidhi vigezo na kwamba DAWASA ilitakiwa kuomba ufafanuzi, DAWASA ilieleza kuwa haikuwa na wajibu wa kutafuta ufafanuzi kama alivyodai Mrufani. Wajibu wa kutafuta ufafanuzi umeelekezwa kwa mlalamikaji kulingana na Sheria ya Ununuzi wa Umma. Hivyo, Mrufani alitakiwa kutafuta ufafanuzi kama aliona kuwa baadhi ya masharti ya zabuni hayakuwa wazi.

DAWASA aliongeza kuwa, alikusudia kutoa zabuni kwa Junaco (T) Ltd ambaye alionesha kuwa na zabuni ya bei ya chini kulingana na nyaraka ya zabuni. Alisema kuwa mlalamikaji hakupendekezwa kupata zabuni kwa sababu hakuzingatia vigezo vilivyotolewa katika nyaraka ya zabuni.

Ili kubaini misingi ya rufaa, Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) ilipitia rufaa hiyo na kugundua kuwa Hati ya Kusudio la kutoa tuzo (Notice of Intension to award) ilionesha kuwa zabuni ya Mrufani ilifutwa kwa sababu haikuwa zabuni yenye bei ya chini katika hatua ya tathmini ya kifedha. Ila baada ya Mamlaka ya Rufani kupitia tathmini ya zabuni ilibaini kuwa zabuni ya Mrufani iliengulіwa katika mchakato wa zabuni kwenye hatua ya awali ya tathmini ya kibiashara kwa kuwasilisha dhamana ya benki ambayo haikukidhi vigezo vilivyoainishwa katika nyaraka ya zabuni.

Mamlaka ya Rufani ilibaini kuwa Dhamana ya Benki ya mlalamikaji ilikuwa halali hadi tarehe 1 Julai 2024, wakati uhalali wake ulipaswa kuwa hadi tarehe 30 Oktoba 2024. Hivyo, Dhamana ya Benki ya mlalamikaji ilikuwa chini ya siku 148. Kwa hiyo, mlalamikaji alifutwa kwa haki kwa kutoa Dhamana ya Benki ambayo ilikiuka masharti ya nyaraka ya zabuni.

Mamlaka ya Rufani ilibaini kuwa kufutwa kwa zabuni ya mlalamikaji ilikuwa halali kwani haikukidhi masharti ya nyaraka ya zabuni. Hivyo kufutwa kwa zabuni ya Mrufani kulifuata matakwa ya Sheria ya Ununuzi na Kanuni zake.

Mamlaka ya Rufani ilitupilia mbali Rufaa ya Mlalamikaji kwa kukosa mashiko na kuiamuru DAWASA kuendelea na mchakato wa zabuni kwa kuzingatia matakwa ya sheria.

# PPAA yapewa kongole kuanzisha moduli ya Kushughulikia malalamiko, rufaa kieletroniki

**KATIBU Tawala Mkoa wa Arusha, Bw. Missaile Musa ameipongeza Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) kwa kuanzisha Moduli ya kuwasilisha na kushughulikia malalamiko na rufaa kwa njia ya kielektroniki katika Mfumo wa Ununuzi wa Umma (NeST).**

Bw. Musa ametoa pongezi hizo alipotembelea banda la PPAA katika maonesho yaliyofanyika wakati wa Kongamano la 15 Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi katika viwanja vya Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha (AICC), Desemba 2024, jijini Arusha.

Aidha, Bw. Musa amefahamishwa majukumu na mafanikio ya PPAA kwa kipindi cha miaka takribani minne chini ya uongozi imara wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.




*Katibu Tawala Mkoa wa Arusha, Bw. Missaile Musa akizungumza na watumishi wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma, (PPAA) alipotembelea banda la mamlaka hiyo wakati Kongamano la 15 Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi lililofanyika katika viwanja vya Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha (AICC), jijini Arusha. Bw. Musa alishiriki kufunga rasmi kongamano hilo lililoanza tarehe 17 – 19 Desemba, 2024.*



*Katibu Tawala Mkoa wa Arusha, Bw. Missaile Musa akikabidhi tuzo ya udhamini na ushiriki wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), katika Kongamano la 15 la Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi kwa Mkuu wa Sehemu ya Huduma za Sheria wa PPAA, Bi. Agnes Sayi wakati wa kufunga kongamano hilo tarehe 19 Desemba 2024. Bi Sayi alipokea tuzo hiyo kwa niaba ya Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando. Kongamano hilo liliandaliwa na Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB).*



*Katibu Tawala Mkoa wa Arusha, Bw. Missaile Musa akiangalia moja ya vipeperushi vya Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), alipokuwa katika banda la mamlaka hiyo wakati Kongamano la 15 la Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi lililofanyika katika viwanja vya Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha (AICC), jijini Arusha.*

# PPAA yashiriki maonesho kongamano la 15 la wataalamu ununuzi, ugavi

**MAMLAKA ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) imeshiriki katika Kongamano la 15 la Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi jijini Arusha.**

Pamoja na mambo mengine, PPAA imetumia fursa hiyo kutoa elimu kwa wadau wa ununuzi walioshiriki kongamano hilo.

Kongamano hilo la siku tatu (3) limeratibiwa na Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB) na limefanyika kuanzia tarehe 17 – 19 Desemba, 2024 jijini Arusha na kuhudhuriwa na washiriki zaidi ya 2,600.

Katika kongamano hilo, PPAA imeshiriki kufanya maonesho na kutoa elimu kuhusu majukumu, malengo na mafanikio yake kwa umma na wadau wa sekta ya ununuzi.

Kongamano limewakutanisha wadau mbalimbali wa sekta ya ununuzi wa umma, wajumbe wa bodi za zabuni, wahandisi, wakaguzi, watafiti, wajasiriamali, wafanyabiashara, wakandarasi na wadau wengine wote wa mnyororo na PPAA.

Wadau hao wamepata fursa ya kujadili na kubadilishana uzoefu katika sekta ya ununuzi wa umma.

Aidha, taasisi zinazosimamia sekta ya ununuzi wa umma nchini nazo zimepata fursa ya kunadi huduma zake na fursa zinazotolewa. Taasisi hizo ni PPAA, Mamlaka ya Udhibiti ya Ununuzi wa Umma (PPRA), Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini (GPSA) na Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB).

Kongamano hilo limewakutanisha wadau wa ununuzi zaidi ya 2,600 limeongozwa na kaulimbiu isemayo: "Procurement and Supply Chain Transformation for Effective Management of Resources" (Mabadiliko ya Ununuzi na Mnyororo wa Ugavi kwa Usimamizi Bora wa Rasilimali).




*Kamishna wa Sera ya Ununuzi Dkt. Fredrick Mwakibinga akisaini kitabu cha wageni wakati alipotembelea banda la PPAA wakati wa Kongamano la 15 la Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi lililofanyika jijini Arusha tarehe 17 - 19, Desemba 2024.*




*Mmoja wa washiriki wa Kongamano la 15 la Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi akipata elimu kuhusu shughuli za PPAA alipotembelea banda la mamlaka hiyo jijini Arusha. Kongamano hilo lilianza tarehe 17 - 19, Desemba 2024.*

# PPAA yamzawadia mhitimu bora wa ununuzi TIA mil 1/-

**MAMLAKA ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) imemzawadia Shilingi milioni moja mhitimu bora wa fani ya manunuzi kutoka Chuo cha Uhasibu Tanzania (TIA) kwa kutambua mafanikio na juhudi za kisomi na ufanisi katika fani ya ununuzi kwa mwaka wa masomo 2023/2024.**

Zawadi hiyo imekabidhiwa kwa mwanafunzi huyo katika Mahafali ya 22 ya chuo hicho yaliyofanyika Desemba 2024 Kampasi ya Dar es Salaam katika viwanja vya TIA.

Akikabidhi zawadi hiyo kwa niaba ya Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando, Mkuu wa Sehemu ya Huduma za Sheria, Bi. Agnes Sayi amesema kuwa lengo la kutoa zawadi hiyo ni kutoa motisha kwa wanafunzi wote wa fani ya Ununuzi na Ugavi kufanya vizuri zaidi.

"Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma imejizatiti kuendelea kutoa motisha kwa wanafunzi wanaofaulu/kufanya vizuri katika fani ya ununuzi na ugavi ili kuweka ushindani wa kufanya vizuri kwa wanafunzi wa fani hiyo," amesema Bi. Sayi.

Kwa upande wake, mwanafunzi aliyefanya vizuri na kupewa kiasi hicho cha fedha Bw. Augustino Komie ameipongeza Mamkala ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) kwa kumzawadi zawadi hiyo na kuongeza kuwa imemfanya kuwa na motisha wa kufanya vizuri zaidi katika masomo yake ya ngazi ya juu na kazini pia.

Naye Naibu Katibu Mkuu Huduma za Hazina, Wizara ya Fedha, Jenifa Christian Omolo, aliyemwakilisha Waziri wa Fedha, Dkt. Mwigulu Nchemba, akizungumza katika mahafali hayo aliipongeza TIA kwa juhudi zake za kukuza elimu na kuhimiza wahitimu kutumia maarifa yao katika maendeleo ya taifa.

Wahitimu 6,950 walitunukiwa vyeti, wakiwemo wanawake 3,838 na wanaume 3,112.



*Naibu Katibu Mkuu Huduma za Hazina, Wizara ya Fedha, Jenifa Christian Omolo.*




*Mkuu wa Sehemu ya Huduma za Sheria, wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), Bi. Agnes Sayi akimkabidhi zawadi mwanafunzi bora wa fani ya Ununuzi kutoka Chuo cha Uhasibu Tanzania (TIA), Bw. Augustino Komie kwa kutambua mafanikio na juhudi za kisomi na ufanisi katika fani ya ununuzi kwa mwaka wa masomo 2023/2024*

# PPAA wanolewa kukabiliana na msongo wa mawazo kazini



*Mwezeshaji wa mafunzo ya kukabiliana na msongo wa mawazo mahali pa kazi, Bi. Zuhura Muro akiendelea kutoa mafunzo kwa watumishi wa PPAA katika ofisi za PPAA jijini Dodoma.*

**KATIKA jitihada za kukabiliana na changamoto ya afya ya akili mahali pa kazi, watumishi wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) wamepatiwa mafunzo ya siku mbili kuhusu njia za kukabiliana na msongo wa mawazo mahali pa kazi.**

Akifungua mafunzo hayo jijini Dodoma, Katibu Mtendaji wa PPAA Bw. James Sando amewasihi watumishi wa Mamlaka ya Rufani kutumia mafunzo hayo kama chachu ya kuongeza tija na ufanisi kazini.

"Kama mtakumbuka siku za hivi karibuni tumefanya baadhi ya mabadiliko hususan kujenga moduli ya kupokea malalamiko na rufaa......lakini pia tutaendelea kufanya mabadiliko katika taasisi yetu ili kutuwezesha kuendana na sayansi na teknolojia, hivyo mafunzo haya ni muhimu kwetu kutujenga kifikra na kutupa mawazo chanya tunapokuwa tunatekeleza majukumu yetu ya kila siku," amesema Bw. Sando.

Pamoja na mambo mengine, Bw. Sando amesema kuwa kupitia mafunzo hayo anaamini kuwa watumishi wataboresha utendaji kazi wao, kuelewa njia za kujitawala na kutawala wengine wakati wa utekelezaji wa majukumu sehemu ya kazi.

Kwa upande wake mwezeshaji wa mafunzo hayo, Bi. Zuhura Muro, amewaasa watumishi kujitahidi wanapokuwa kazini kufanya kazi kwa kuzingatia utu, kanuni na taratibu za kazi ili kuepuka migogoro isiyo na lazima kazini.

"Lengo kuu la nyie kuwa hapa ni kuisaidia Serikali kutekeleza majukumu yake kwa wakati na ufanisi, sasa inapoibuka migogoro sehemu ya kazi, husababisha baadhi ya watumishi kupatwa na msongo wa mawazo na kushindwa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi, hivyo kupitia mafunzo haya kila mmoja ataweza kuelewa anapopaswa kujirekebisha ili kuongeza ufanisi," amesema Bi. Muro

Akielezea kuhusu akili hisia, Bi. Muro ameongeza kuwa utumiaji wa akili hisia kazini na jinsi mtumishi anavyotumia hisia kwa busara ili kumwezesha kupata matokea chanya ambayo humsaidia mtumishi husika kuipenda kazi yake na kuboresha ufanisi katika kutekeleza majukumu yake.

"Wakati mwingine mtumishi anakumbwa na matatizo ya kifamilia inamsababishia kuwa na msongo wa mawazo, hasa ukizingatia mtumishi anapokuwa kazini muda mwingi anautumia kuwa kazini lakini endapo ana msongo wa mawazo atashindwa kutekeleza majukumu yake kwa wakati na ufanisi," ameongeza Bi. Muro.

Mada zilizowasilishwa wakati wa mafunzo hayo ni pamoja na kujitambua wewe ni nani, uongozi binafsi, akili hisia kwa mafanikio ya maisha na kazi, ustahimilivu kazini, msongo wa mawazo na afya ya akili.



*Katibu Mtendaji wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), Bw. James Sando, (aliyekaa katikati), Mwezeshaji wa mafunzo ya kukabiliana na msongo wa mawazo mahali pa kazi, Bi. Zuhura Muro (aliyekaa kushoto) na Meneja wa Huduma za Mamlaka ya Rufani, Bw. Paschal Kajuna katika picha na watumishi walioshiriki mafunzo ya njia za kukabiliana na msongo wa mawazo kazini katika ofisi za PPAA jijini Dodoma.*

PUBLIC PROCUREMENT APPEALS AUTHORITY
BULLETIN
UTOAJI RUFAA KWA UFANISI NA HAKI
PPAA
Toleo Na: 03 Oktoba - Desemba 2024

# PPAA na falsafa ya R4 katika kuimarisha utoaji haki



## Zaongeza uwazi, uwajibikaji wa zabuni za umma

**MAMLAKA ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) ni taasisi iliyo chini ya Wizara ya Fedha iliyoundwa kwa mujibu wa Sheria ya Ununuzi ya Umma Na. 3 ya Mwaka 2001 ambapo baada ya sheria hiyo kufutwa, Mamlaka ya Rufani ilihuishwa chini ya Sheria ya Ununuzi ya Umma Na. 21 ya Mwaka 2004.**

Aidha Mamlaka ya Rufani ilihuishwa tena kupitia Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 7 ya Mwaka 2011 baada ya Sheria Na. 21 ya Mwaka 2004 nayo kufutwa. Mwaka 2023 Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 7 ya Mwaka 2011 nayo ilifutwa na Mamlaka ya Rufani ilihuishwa tena kupitia Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 10 ya Mwaka 2023.

Kwa mujibu wa sheria hiyo, jukumu kuu la PPAA ni kupokea, kusikiliza na kutoa maamuzi ya malalamiko au rufaa zitokanazo na maamuzi ya maafisa masuuli wa taasisi mbalimbali za umma katika michakato ya ununuzi wa umma. Pia, ina jukumu la kupokea na kusikiliza malalamiko ya wazabuni ambao hawakuridhishwa na uamuzi wa kufungiwa (blacklist) na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA).

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa Awamu ya Sita chini ya uongozi imara wa Rais Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imeendelea kudumisha misingi ya utawala bora ikiwemo haki na usawa, pamoja na kuendelea kusimamia miradi ya kimkakati yenye tija kwa nchi na hivyo kuiwezesha serikali kupata thamani halisi ya fedha katika ununuzi wa umma.

> “Katika kipindi cha uongozi wa Rais Mhe. Dkt. Samia, PPAA imeendelea kutekeleza jukumu lake kuu la utatuzi wa migogoro itokanayo na michakato ya ununuzi wa umma kwa haki, uwazi, uadilifu na kwa muda mfupi ili kuwezesha upatikanaji wa thamani halisi ya fedha na kufikia malengo ya kutoa huduma bora kwa wananchi kwa wakati.”

Kwa kuwa takribani asilimia 70 ya Bajeti ya Serikali hutumika kwa ajili ya ununuzi wa umma, sheria, kanuni na miongozo ya ununuzi wa umma zinaiwezesha serikali kuendelea kuimarisha sekta ya ununuzi.

Katika kipindi cha uongozi wa Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, PPAA imeendelea kutekeleza jukumu lake kuu la utatuzi wa migogoro itokanayo na michakato ya ununuzi wa umma kwa haki, uwazi, uadilifu na kwa muda mfupi ili kuwezesha upatikanaji wa thamani halisi ya fedha na kufikia malengo ya kutoa huduma bora kwa wananchi kwa wakati.

PPAA chini ya Uongozi imara wa Mhe. Rais Samia imefanikiwa katika maeneo ya falsafa ya R nne (4R) za Mhe. Dkt. Samia

*Inaendelea Uk 9*

Inatoka Uk 8

# PPAA na falsafa ya R4 katika kuimarisha utoaji haki

Suluhu Hassan kama ifuatavyo: -

**i. Usuluhishi wa Migogoro (Reconciliation)**

PPAA imeweza kushughulikia jumla ya mashauri 162 yaliyotokana na michakato ya ununuzi wa umma. Aidha, katika mashauri hayo, PPAA ilizuia utoaji tuzo kwa zabuni 35 zenye thamani ya takribani TZS. 583,591,615,609.00 kwa wazabuni wasio na uwezo wa kifedha pamoja na wale waliokosa sifa za kitaalamu za kutekeleza zabuni husika. Hatua hii iliepusha utekelezaji usioridhisha wa miradi unaosababisha upotevu wa fedha za umma na kuchelewesha maendeleo stahiki kwa wananchi.

Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Dkt. Samia inaamini kuwa usuluhishi wa migogoro hauwezi kupatikana penye ubaguzi na pale ambapo kuna wanaokosa fursa na haki zao za kiuchumi na kiraia. Hivyo, kitendo cha PPAA kuzuia utoaji wa tuzo kwa wazabuni 32 waliokosa sifa kinaweka uzito katika usuluhishi wa migogoro ambayo ni moja ya falsafa za Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.



PPAA imeendelea pia kudhibiti taasisi nunuzi kukiuka taratibu za kisheria hasa katika kufanya tathmini ya zabuni (tender evaluation); katika baadhi ya mashauri, PPAA ilifanikiwa kubaini ukiukwaji wa taratibu za kufanya tathimini uliofanywa na taasisi nunuzi ikiwemo kutokuzingatia vigezo vilivyowekwa katika kabrasha la zabuni au kuongeza vigezo vipya ambavyo havikuwepo awali.

**ii. Mageuzi (Reform)**

Serikali ya Awamu ya Sita imewezesha kutungwa upya kwa Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2023 na kuruhusu hatua za mageuzi kuchukuliwa pale ambapo ilibainika kuwa kulikuwa na ukiukwaji wa taratibu katika mchakato wa ununuzi. Kupitia Sheria Mpya ya Ununuzi wa Umma mageuzi mbalimbali yalifanyika yakiwemo: -

**a)** Kupunguza muda wa ushughulikiaji malalamiko au rufaa zinazotokana na michakato ya ununuzi wa umma. Mfano, muda wa siku saba (7) za kazi kwa ajili ya kusubiri malalamiko ya wazabuni (cool off period) kabla ya kutoa tuzo umepunguzwa na kuwa siku tano (5) za kazi. Muda huo hautajumuisha njia za ununuzi ambazo hazihitaji ushindani ambazo ni single source, minor value procurement na shopping; muda wa Afisa Masuuli kushughulikia malalamiko ya zabuni pia umepunguzwa kutoka siku saba (7) za kazi hadi siku tano (5) za kazi na pale ambapo Afisa Masuuli ataunda jopo la mapitio malalamiko basi atakuwa na siku saba (7) za kazi za kushughulikia na atatakiwa kuwajulisha washiriki wa zabuni kuwepo kwa jopo; na muda wa PPAA kushughulikia malalamiko au rufaa kutoka siku arobaini na tano (45) hadi siku arobaini (40).

**b)** Kuweka masharti ya lazima kwa taasisi nunuzi kufanya ununuzi kupitia mfumo wa kieletroniki. PPAA imefanikiwa kuanzisha moduli mpya ya kuwasilisha rufaa/malalamiko kwa njia ya kieletroniki (Complaint & Appeal Management). Moduli hiyo inarahisisha uwasilishaji wa malalamiko na kutoa fursa kwa wazabuni wengi zaidi kuwasilisha malalamiko yao. Aidha, moduli hiyo ni rafiki na inaokoa muda wa kuwasilisha malalamiko. Moduli ya Complaint & Appeal Management imewekwa kwenye Mfumo wa Ununuzi wa Umma Kieletroniki (NeST), uliojengwa chini ya Uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita.

Aidha, mafunzo ya siku mbili kuhusu moduli ya uwasilishaji wa malalamiko/rufaa kwa njia ya kieletroniki yaliandaliwa na Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) kwa kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) kwa taasisi nunuzi na wazabuni takribani 350 wa mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Morogoro na Pwani yalifanyika jijini Dar es Salaam tarehe 29 na 30 Mei, 2024.

**iii. Kujenga upya (rebuild)**

Serikali ya Awamu ya Sita imewezesha na kuboresha usimamizi wa sekta ya ununuzi wa umma nchini, hatua ambayo imeiwezesha PPAA kuwajengea uwezo wajumbe wa mamlaka na watumishi wake na kuboresha mazingira ya kazi kwa kuwapatia vifaa muhimu katika utekelezaji wa majukumu ya PPAA na kuiwezesha serikali kufikia malengo yaliyokusudiwa kwa wakati na kupata thamani halisi ya fedha katika ununuzi wa umma.

**iv. Ustahimilivu (Resilience)**

Licha ya athari za kiuchumi zilizoikumba na zinazoendelea kuikumba dunia na kutikisa uchumi kama Covid-19, vita ya Urusi na Ukraine pamoja na kuadimika kwa fedha za kigeni (USD), bado Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeendelea kuiwezesha PPAA kustahimili athari hizo na kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Katika jitihada za kuhakikisha kuwa taasisi nunuzi na wazabuni wanatumia mfumo wa ununuzi NeST, kama ilivyoelekezwa kwenye Sheria ya Ununuzi, PPAA imeanza kufanya tathimini ya kutumia Moduli ya kupokea na kuwasilisha malalamiko na rufaa (User Acceptance Test) kieletroniki katika Mfumo wa Ununuzi wa Umma Kieletroniki (NeST) mwezi Septemba 2024, jijini Dodoma.

Kufanyika kwa tathmini hiyo ni ishara kuwa muda si mrefu moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko itaanza rasmi kutumika kama ilivyokuwa imekusudiwa. Moduli hiyo ina faida kadhaa ambazo ni pamoja na kuokoa muda na kupunguza gharama zilizokuwa zikiingiwa wakati wa uwasilishaji wa rufaa na majibu ya hoja za rufaa. Pia itawezesha wahusika katika shauri kuweza kufuatilia na kufahamu hatua zote za uchakataji wa shauri unavyoendelea.

# PPAA yatupa rufaa dhidi ya Muhimbili, haina mashiko

**MAMLAKA ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) imepinga rufaa iliyowasilishwa dhidi ya Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH)** kwa kukosa mashiko na kuamuru Muhimbili kuendelea na zabuni kwa kuzingati sheria ya ununuzi wa umma.

Rufaa hiyo iliwasilishwa na Kampuni ya Nimaco Tanzania Ltd baada ya kutoridhishwa na sababu zilizotolewa za kuitoa nje kwenye zabuni ya Utoaji wa Huduma za Ulinzi hospitalini hapo.

Nimaco Tanzania Ltd alieleza kuwa tarehe 24 Septemba 2024, alipokea barua kutoka MNH ikieleza kuwa zabuni yake haikukidhi vigezo katika hatua ya tathmini ya kutimiza masharti (post-qualification stage) kwa sababu ya utendaji mbaya katika mkataba wake wa wakati huo.

Mlalamikaji alisema anapinga kuenguliwa kwake katika hatua ya tathmini ya baada ya kutimiza masharti kwa sababu ya kutumia sababu ambayo haikuwa sehemu ya masharti yaliyotolewa katika nyaraka ya zabuni.

Mlalamikaji alisisitiza kuwa yeye ni mtoa huduma wa sasa (previous service provider) katika ofisi ya mlalamikiwa na kipindi chote cha mkataba huo, hajawahi kupokea barua ya onyo kutoka kwa mlalamikaji ambayo inaonesha kutoridhika kwake na huduma alizozitoa.

Nimaco Tanzania Ltd aliendelea kueleza kuwa mwishoni mwa mwaka 2022, alipokea barua kutoka MNH ambazo zilimtaka kutekeleza masharti ya mkataba, ikiwemo kulipa mishahara ya walinzi waliokuwa wakifanya kazi kwa wakati.

Alidai walinzi ambao hawakulipwa walikuwa na mgogoro na yeye baada ya kufukuzwa kazi na kudai baada ya kupewa mkataba (wa sasa) wakati huo, walinzi hao wa mtoa huduma wa awali walimlazimisha yeye kuwaajiri tena kama sehemu ya masharti ya mkataba.

Mlalamikaji alidai alikubali kuwaajiri walinzi hao kama alivyotakiwa na mlalamikiwa lakini walishindwa kutii masharti na hali za ajira zao hivyo alilazimika kuwafukuza kazi. Kutokana na kufukuzwa kazi, walinzi hao wamekuwa wakimtumia barua nyingi mlalamikiwa kwa lengo la kuharibu sifa ya Kampuni ya Nimaco Tanzania Ltd.

Alieleza baada ya kupokea barua kutoka kwa mlalamikiwa iliyotaka malipo ya madeni ya mishahara ya walinzi, aliingia katika makubaliano maalumu na walinzi hao kuhusu njia ya kulipa madeni hayo na alitekeleza malipo kama walivyokubaliana.

Alieleza kuwa kitendo chake cha kulipa madeni ya mishahara kwa baadhi ya walinzi ambao walikuwa na mgogoro kuhusu kufukuzwa kwao kazi hakiwezi kuhesabiwa kama utendaji mbaya kama inavyodaiwa na MNH.

Aidha, alieleza zaidi kwamba wakati wa utekelezaji wa mkataba wa sasa (wakati huo), ucheleweshaji katika kulipa mishahara pia ulichangiwa na kitendo cha mlalamikiwa kuchelewa kufanya malipo ya kila mwezi kwa kazi iliyofanywa na mlalamikaji.

Kutokana na hilo, mlalamikaji alidai ucheleweshaji wa malipo kwa MNH wakati mwingine ulifikia hadi miezi mitatu na kuchangia mlalamikaji kushindwa kufanya malipo ya mishahara kwa walinzi wake kwa wakati.

Pia alilazimika kutafuta vyanzo vingine vya mapato kutekeleza malipo hayo. Hivyo, MNH ilichangia kushindwa kwa Nimaco Tanzania Ltd kufanya malipo ya mishahara kwa wakati. Kwasababu hiyo, mlalamikaji hakupaswa kuadhibiwa kwa sababu hali hiyo ilichangiwa pia na mlalamikiwa.

Mlalamikaji alieleza mbali na ucheleweshaji wa malipo ya mishahara, kulingana na mlalamikiwa, zabuni ya mlalamikaji haikukubaliwa katika hatua ya tathmini ya baada ya kutimiza masharti (post-qualification) kutokana na kutokuwepo kwa walinzi katika baadhi ya maeneo ya ulinzi na ilisababisha changamoto kadhaa ikiwemo kutoroka kwa wagonjwa.

Alikataa dai la mlalamikiwa kuhusu suala hilo kwani hajawahi kupokea onyo kutoka kwa mlalamikiwa kuhusu kutoroka kwa wagonjwa. Zaidi ya hayo, kutokana na asili ya MNH, ni vigumu kutambua wagonjwa waliolazwa, wa nje, na watu wengine kwa sababu hakuna mavazi maalumu kwao.

Mlalamikaji aliongeza hakukuwa na mahitaji katika mkataba wa sasa (wakati huo) kumtaka mlalamikaji kuhakikisha wagonjwa hawatoroki kutoka katika majengo hospitali. Hivyo, mlalamikaji alidai kitendo cha mlalamikiwa kumuengua katika zabuni hiyo hakikuwa cha haki.

Kuhusu kutokuwepo kwa walinzi, mlalamikaji alieleza katika baadhi ya maeneo ya ulinzi, walinzi walitakiwa kuwa kwenye vituo vyao kwa saa 12 na katika maeneo mengine kwa saa 24. Alidai alizingatia mahitaji hayo kwa kuhakikisha walinzi walikuwa wanapatikana kwenye vituo vyao kama ilivyobainishwa. Hivyo, alikanusha kuwepo kwa tatizo la kutokuwepo kwa walinzi kama ilivyodaiwa.

Alipoulizwa na wajumbe wa PPAA kuhusu makato yaliyofanyika kwenye malipo ya kila mwezi kwa Mei, Juni na Julai 2023, mlalamikaji alikubali makato yalifanyika kipindi hicho kutokana na kutokuwepo kwa walinzi katika baadhi ya maeneo ya ulinzi. Mlalamikaji alieleza baada ya kugundua kwamba kulikuwa na makato kwenye malipo ya kila mwezi, alifanya ufuatiliaji usio rasmi kwa mlalamikiwa na hakukuwa na malalamiko ya maandishi yaliyowasilishwa. Mlalamikaji alichukua hatua hiyo ili kudumisha uhusiano mzuri na mlalamikiwa licha ya makato hayo kuwa si halali.

Mlalamikaji alieleza uamuzi wa MNH wa kumuengua katika mchakato wa zabuni ulitokana na ripoti ya ulinzi ambayo iliandaliwa na mlalamikiwa peke yake. Mlalamikaji alidai hakuwahi kupewa ripoti hiyo wakati wa kipindi chote cha mkataba. Alisema kawaida, katika ofisi nyingine anazotoa huduma zinazofanana, ripoti ya ulinzi kabla ya kuzingatiwa kuwa ya mwisho, hupitiwa na kujadiliwa na pande zote mbili.

Hata hivyo, alieleza haikuwa hivyo katika ofisi ya mlalamikiwa ndio maana mlalamikaji anashuku kuwa ripoti ya ulinzi iliyotayarishwa na mlalamikiwa na kutumika kama msingi wa kumuengua katika mchakato wa zabuni kwa njia isiyofaa.

Alieleza kama angekuwa na utendaji mbaya wakati wa utekelezaji wa mkataba, mlalamikiwa asingekubali kuongeza muda wa mkataba wake mara tatu. Alieleza hatua ya MNH kuongeza muda wa mkataba wake hadi tarehe 31 Oktoba 2024 kutoka tarehe 30 Julai 2024, inaonesha alikuwa ameridhika na utendaji kazi wake. Hivyo, mlalamikaji anastahili kupata tuzo ya zabuni kwani kitendo cha kumuondoa kilikuwa kinyume na sheria za ununuzi wa umma.

Kwa upande wake, MNH ilieleza wakati wa tathmini, wakati

# PPAA yatupa rufaa dhidi ya Muhimbili, haina mashiko

wa mchakato wa (post-qualification), zabuni ya mlalamikaji iligundulika kutokuwa sahihi kutokana na utendaji mbaya katika mkataba wa sasa (wakati huo).

Muhimbili iliongeza kuwa mlalamikaji ndiye mtoa huduma wa sasa katika ofisi ya mlalamikiwa na kwamba wakati wa utekelezaji wa mkataba wa sasa, kulikuwa na changamoto kadhaa zilizoshuhudiwa upande wa mlalamikaji, zilijumuisha kuchelewa kwa malipo ya mishahara ya walinzi waliopo kazini na kutohudhuria kwa walinzi kwenye vituo vya kazi na kusababisha wagonjwa kutoroka na wizi wa vifaa vya hospitali.

Muhimbili ilieleza kutokana na utendaji mbaya wa mlalamikaji, walimtumia barua kadhaa kumkumbusha kuzingatia masharti ya mkataba na kutekeleza wajibu wake ipasavyo.

Aidha, Muhimbili ilisema licha ya barua za onyo zilizotumwa kwa mlalamikaji, changamoto ya kutohudhuria walinzi iliendelea kiasi kwamba Muhimbili iliamua kupunguza malipo ya kila mwezi ya mlalamikaji kwa Mei, Juni na Julai 2023.

Hata hivyo, mlalamikaji hakupinga mapungufu yaliyofanywa, na inathibitisha utendaji mbaya wa mlalamikaji.

Kuhusu kutohudhuria kwa walinzi katika baadhi ya vituo, Muhimbili ilieleza kulingana na ratiba ya mahitaji, mlalamikaji alitakiwa kutoa huduma za ulinzi kwa saa 24 katika vituo vyote.

Hivyo basi, madai ya mlalamikaji kwamba katika baadhi ya vituo walinzi walipaswa kuwepo kwa saa 12 tu, inaonesha mlalamikaji alikosea kuelewa mahitaji. Aidha, alieleza kuwa kutokana na aina ya kazi za Muhimbili, mtoa huduma ya ulinzi alipaswa kutoa huduma za ulinzi kwa saa 24.

Kuhusu hoja ya mlalamikaji kwamba ripoti ya ulinzi iliandaliwa na mlalamikiwa pekee, hivyo kuhusisha taarifa zilizopotosha, Mkuu wa Idara ya Huduma za Ulinzi wa Muhimbili alieleza kwamba ripoti hiyo huandaliwa kwa kukusanya taarifa zilizopo kwenye daftari la usajili wa mahudhurio.

Alisema walinzi wanasaini daftari la mahudhurio kila siku baada ya kuripoti kwenye vituo vya kazi. Daftari la mahudhurio lina taarifa kuhusu idadi ya walinzi waliopo kwenye vituo vya kazi kila siku.

Mlalamikiwa hufanya mchakato wa kuunganisha taarifa zilizomo kwenye daftari la mahudhurio anapokuwa anaandaa ripoti ya ulinzi, hivyo, alidai hoja ya mlalamikaji kwamba ripoti ya usalama ya mlalamikiwa imetengenezwa kwa nia mbaya, haina mashiko kwani taarifa zote zilizopo kwenye ripoti hiyo zinatokana na daftari la mahudhurio.

Muhimbili ilipinga hoja ya mlalamikaji kwamba ilichelewa kufanya malipo ya kila mwezi na kuongeza kuwa imekuwa ikilipa kila mwezi kwa wakati ambapo licha ya kulipwa kwa wakati, mlalamikaji amekuwa akichelewa kulipa mishahara ya walinzi wake, matokeo yake, changamoto ya kutohudhuria kazini kwa walinzi iliendelea. Hivyo, Muhimbili iliomba PPAA kutozingatia hoja ya mlalamikaji kuhusu kuchelewa kwa malipo.

Katika kuamua msingi wa rufaa, PPAA ilikagua sehemu IV: Vigezo (Qualification and Evaluation Criteria) na Tathmini ya Zabuni na ilibaini mahitaji kadhaa ambayo yalipaswa kuzingatiwa wakati wa tathmini ya zabuni.

Miongoni mwa vigezo vilivyotajwa ni pamoja na uzoefu, hasa uzoefu maalumu. Kwa uzoefu maalumu, waombaji zabuni walitakiwa kuonesha kama wamemaliza kwa kuridhisha na kwa kiasi kikubwa mkataba wa aina sawa na huo kuanzia tarehe 1 Januari 2021 hadi tarehe 31 Desemba 2023.

Katika kuhakikisha kama mlalamikaji alikidhi mahitaji yaliyotajwa hapo juu, PPAA ilikagua zabuni ya mlalamikaji kwenye mfumo wa NeST na kubaini mlalamikaji aliorodhesha mikataba mitatu tofauti kama uthibitisho wa uzoefu maalumu.

Mikataba hii ilikuwa na taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam (DIT), Malawi Cargo Ltd na MNH. Mikataba hii ilikuwa ndani ya kipindi kilichotajwa na kila moja ilikuwa na thamani inayozidi TZS 100,000,000 kama ilivyoainishwa kwenye Nyaraka ya Zabuni.

PPAA ilibaini wakati wa tathmini zabuni ya mlalamikaji iligundulika kuwa zabuni iliyo na bei nafuu zaidi baada ya kuzingatia mahitaji yaliyotajwa kwenye nyaraka ya zabuni. Baada ya kubaini zabuni ya mdaiwa ilikuwa zabuni iliyo na bei nafuu zaidi kulingana na taarifa zilizotolewa katika mfumo wa NeST, mdaiwa alifanyiwa mchakato wa uhitimu (post-qualification).

Kulingana na rekodi ya rufaa, mlalamikiwa alifanya mchakato wa uhitimu ili kuthibitisha ukweli wa taarifa za mlalamikaji zilizotolewa katika mfumo wa NeST. Ripoti ya mchakato wa uhitimu inaonesha wakati wa utekelezaji wa mkataba wa sasa, mlalamikiwa aligundulika kuwa na mapungufu kadhaa, ikiwemo kutohudhuria kwa walinzi kwenye vituo vya kazi, mlalalamikaji kushindwa kulipa mishahara wafanyakazi wake kwa wakati, na kitendo cha walinzi kuacha vituo vya kazi bila uangalizi.

PPAA ilibaini mlalamikiwa alikuwa ameandika barua kadhaa kwa mlalamikaji zikionesha kutoridhika na huduma alizotoa. Muhimbili kupitia barua yake ya tarehe 3 Oktoba 2024 kwa mlalamikaji alieleza mapungufu hayo ya Mei, Juni, na Julai 2023 yalitokana na kutohudhuria kwa walinzi wa mlalamikaji kwenye vituo vya kazi.

PPAA ilizingatia zaidi hoja ya mlalamikaji kuhusu kutohudhuria kwa walinzi kwenye vituo vya kazi. Mlalamikaji alidai kuwa kulikuwa na baadhi ya vituo vya kazi ambavyo walinzi hawakuhitajika kuwa na huduma za saa 24. PPAA ilikagua mkataba wake na ilibaini Kifungu cha 1 cha ratiba hiyo kilisema kwa uwazi kuwa mlalamikaji alipaswa kutoa huduma za ulinzi kwa saa 24. Hakukuwa na kifungu kilichosema katika baadhi ya vituo huduma za ulinzi zilihitajika kwa saa 12 tu kama alivyodai mlalamikaji.

PPAA ilizingatia pia hoja ya mlalamikaji kwamba ripoti ya usalama ambayo mlalamikiwa alitumia kumuengua kwenye zabuni wakati wa mchakato wa uhitimu ilikuwa imepitishwa kwa nia mbaya. Baada ya kupitia rekodi ya rufaa na hoja za pande zote, PPAA ilibaini kuenguliwa kwa zabuni ya mlalamikaji hakukuzingatia tu ripoti ya usalama, bali pia kulitegemea ushahidi mwingine kama barua za onyo, mapungufu kwenye malipo, na kukiri kwa mlalamikaji kuhusu kutohudhuria kwa walinzi kwenye vituo vya kazi.

Kwa kuzingatia maelezo hayo, PPAA imehitimisha kwamba utendaji kazi wa mlalamikaji katika mkataba wa sasa haukuridhisha. Kwa mazingira hayo, PPAA inaona hatua ya Muhimbili kumuengua katika zabuni ilikuwa sahihi na ilizingatia Sheria ya Ununuzi wa Umma. Hivyo, PPAA inatupilia mbali rufaa hiyo kwa kukosa maashiko. Kadhalika, PPAA imeielekeza MNH kuendelea na mchakato wa zabuni kwa kuzingatia Sheria ya Ununuzi wa Umma.

# HABARIPICHA




*Katibu Mtendaji wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), Bw. James Sando akizungumza jambo na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Bw. Godfrey Nyaisa wakati alipotembelea banda la mamlaka hiyo katika Kongamano la 15 la Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi lililofanyika tarehe 17 – 19 Desemba, 2024 jijini Arusha.*




*Mdau wa ununuzi na ugavi akipata maelezo kutoka kwa watumishi wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) kuhusu majukumu mbalimbali ya mamlaka hiyo wakati alipotembelea banda la mamlaka hiyo katika Kongamano la 15 Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi lililofanyika tarehe 17 – 19 Desemba, 2024 jijini Arusha.*




*Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA), Bw. Denis Simba akisaini kitabu cha wageni katika banda la Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) alipotembelea banda la mamlaka hiyo katika Kongamano la 15 Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi lililofanyika tarehe 17 – 19 Desemba, 2024 jijini Arusha.*




*Katibu Mtendaji wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), Bw. James Sando, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA), Bw. Denis Simba wakiteta jambo na Mkurugenzi wa Mafunzo kutoka Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB), Bw. Amos Kazinza katika Kongamano la 15 Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi lililofanyika tarehe 17 – 19 Desemba, 2024 jijini Arusha.*